# Khilafah

RAMADHANI 1447 HIJIRIA —FEBRUARI 2026 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO


## TOLEO MAALUM LA RAMADHANI 1447 HIJIRIA

## KARIBU RAMADHANI : MGENI MTUKUFU ULIYETAKASIKA NA DHIHAKA




Ramadhani imeanza, kama kawaida tutashuhudia dhihaka na dharau za wanademokrasia kwa mgeni huyu adhimu na Uislamu kwa jumla.

Wanasiasa wa kidemokrasia katika madola makubwa kama Marekani,Uingereza, Ufaransa, Canada nk. na nchi changa kama kawaida yao hujifanya kupaza sauti zao ati kutuma salamu za kuwatakia Waislamu kheri ya kuingia Ramadhani. Aidha, hata hapa petu tunawasikia wengi kutoa salamu za Ramadhani Kariim.

Si hayo tu bali pia tutaona maandalizi ya futari kutoka kwa viongozi hao ati kwa ajili ya Waislamu.

Tunasema hii ni dhihaka, dharau na shere kubwa kwa Umma wa Kiislamu na mfumo wake, kwa kuwa madola kama Marekani na washirika wake na hata wafuasi wao katika nchi changa daima wako mbioni kufanya kazi ili kuangamiza Ummah wa Kiislamu

**Inaendelea Uk. 3**

## RAMADHANI CHACHU YA KIMFUMO



Moja katika fadhila kubwa ya mwezi mtukufu wa Ramadhani ni kupatikana ndani yake suala la kuteremshwa Quran, ambayo ni muongozo wa watu, zama na katika kila kipengee cha maisha ya wanadamu.

Allah Taala anasema:

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ

*“Ni mwezi wa Ramadhani ndio ambao imeteremshwa humo Qur’an kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi”*

(TMQ 2:185)

**Inaendelea Uk. 5**

Jarida la Khilafah
Linawatakia Mfungo wa
Mwema Ramadhani
Ya 1447 Hijiria
umma wa Kiislamu
Duniani kote

**Yaliyomo :**


- **Ramadhani itusukume kujiamini**........................................ 2
- **Mama Itumie Vyema Fursa ya Ramadhani** ...............................4
- **Fat-hi ya Andalus** ...................................................................6

## RAMADHANI ITUSUKUME KUJIAMINI NA UISLAMU WETU

Mwezi wa Ramadhani umeanza, mwezi ambao huunganisha Umma wetu mtukufu katika Ibada tukufu ya kufunga ambayo ni nguzo katika nguzo za dini yetu ya Kiislamu.

Hata hivyo, katika mwezi huu ni wajibu tuutanue upeo wetu kinyume na tulivyozoea kuichukulia haiba ya Ramadhani kwamba ni mwezi wa Ibaadat za kiroho tu. ikiwa tutaichukulia Ramadhani kwa mtizamo wa upande mmoja wa Ibaadat za kiroho tu tutakua tunaufanyia dhulma mwezi huu mtukufu. Hii ni kwa sababu Qurani inatukumbusha kwamba mwezi huu ndio iliposhushwa kuwa muongozo kwa watu wote katika kila kipengee cha maisha yetu yote. Pia kwa upande wa pili katika mambo ya muamalati (mjumuiko wa watu) kama kuuziana, utawala, vita, ndoa n.k. Kwa hivyo mwezi huu mtukufu utuharakishe kuubeba msimamo wetu wa asili nao ni kuuchukua Uislamu kama mfumo kamili na bora kwa kila kipengee cha wanadamu wa zama zote.

Tangu kuibuka mfumo batil wa kibepari mwishoni mwa karne ya 18 miladia na kuangushwa Dola ya Kiislamu [Khilafah Uthmania] katika mwaka 1924 [miladi], fikra ya kuitenganisha dini na maisha (secularism) imekuwa ikipigiwa debe na kufanywa ndio kaulimbiu na makafiri, wakala wao katika vibaraka, wanafikra wao kiasi cha kuwachanganya baadhi ya Waislamu na kupelekea kuifanya dini yao kuwa ni dini ya masuala ya Ibaadat tu. **Huu ni msiba mkubwa!** uliowapelekea baadhi ya Waislamu kupoteza thika/kujiamini na kuufanya Uislamu kama dini mithili ya dini nyengine kama ukiristo, ubudha na uhindu. Kuwa ni dini ya kulialia sana kwa kufanya Ibada za kiroho tu bila ya kuwa na masuluhisho yoyote maishani, na badala yake kutegemea ubepari kutatua matatizo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ni wajibu Umma wa Kiislamu kuirejesha thika yao katika upande wa nafsiya (matendo) yao kwa kufanya Ibadat mbalimbali lakini pia kujenga na kuimarisha aqliya (mentality) yao kwa kuubeba Uislamu kama mfumo kamili ulioletwa kumkomboa mwanaadamu.

Hali hii ya kujiamini kwa Umma wetu tutairejesha kwa kuitupia macho tarekhe yetu tukufu ya Kiislamu namna ilivyojaa kila aina ya misimamo na mapambano katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani.

Mtume (S.A.W) na masahaba zake watukufu licha ya kufunga, kuswali na kuomba maghfira katika mwezi huu pia walitoka mchakamchaka kuelekea Badri katika mwezi kama huu kupambana na makafiri.

Pia katika mwaka wa nane wa Hijria mwezi kama huu wa Ramadhani waliizingira Makka na kuikomboa na uchafu wa masanamu na uongozi batil wa kiqureish na kuiweka chini ya Himaya ya Dola la Kiislamu.

Kadhalika Waislamu waliokuja baada yao hawakuichukulia Ramadhani kama mwezi wa kula vitamu vya tunu tu na kumalizia kwa kutaka maghfira pekee bali walisimama kidete kivitendo kuitanua Dola ya Kiislamu kwa kufanya fat-hi mbalimbali na kuulinda ushindi walioupata kwa kusimama msimamo thabiti bila ya kutetereka.

Tukumbuke Jemadari Tariq bin Ziyad aliifungua (Fathi) Spain na Ureno (Andalusia) katika Ramadhani mwaka 93 Hijria, kadhalika jemadari Salahudin Ayoub aliwafurusha makafiri katika vita vya 'Hittin' katika mwaka 584 Hijria, lakini tusisahau pia mapambano makali ya jihadi dhidi ya Mongols katika Vita vya 'Ain-Jaloot' yaliotokea Ramadhani Mwaka 627 Hijiria.

Huu ndio msimamo uliobebwa na Mtume, Masahaba na Waislamu wema waliofuata, nasi lazima tuandame msimamo huo.

Kwa kila mwenye kutaka ukombozi wa Umma huu tuitumie Ramadhani kurejesha msimamo wetu wa kuchanganya ibadaat na siasa ili kurejesha nafasi yetu ya asili kama Umma bora ulioletwa kuukomboa ulimwengu na binaadamu wote kwa jumla.

Mwisho, tunatoa salamu za pongezi kwa Waislamu wa Tanzania na ulimwengu mzima kwa kuanza Ramadhani. Tunamuomba Allah Taala Atupe tawfiq ya kuifunga na kupata malipo yake makubwa. Amiin

**Mhariri**

**Ramadhani 1447 Hijria**

**Februari 2026 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

*************

na mfumo wao. Iweje kuwatakia Waislamu kheri katika ibada ya Ramadhani ilhali kile kinachoilinda na kudhamini ladha na thamani ya Ramadhani ambacho ni dola ya Khilafah wanaipinga kurejea kwake kwa nguvu na gharama zote?

Waislamu pia kupewa salamu za Ramadhani kutoka mabunge ya kidemokrasia na mfano wake ni jambo la kushangaza sana, kwa kuwa imani ya kisekula ya mabunge hayo ya kidemokrasia inapingana moja kwa moja na aqida ya Kiislamu, hasa ukitilia maanani kuwa Ramadhani ni mwezi ulioshushwa muongozo kwa watu wote. (huda li-nasi)

Mfumo wa kibepari na nidhamu yake ya kidemokrasia kamwe hauthamini, haujali wala hauheshimu na hautoheshimu mwezi wa Ramadhani. Wao na mfumo wao ndio huruhusu na kudhamini kila aina ya uchafu na ufuska katika ulimwengu hata ndani ya kipindi cha mwezi mtukufu "mgeni mwema".

Tunashuhudia dhulma zao za kiuchumi, uvamizi wa biladi za Waislamu kama wanavyofanya Syria, Iraq, Somalia, Afghanistan, Sudan na yanayoendelea Gaza, pia na kuunga mkono kwao vibaraka wanaoangamiza Waislamu kama ndani ya Saudia, Turkistan ya Mashariki, Myanmar, Kashmir nk.

Aidha, upinzani wa nchi za magharibi dhidi ya ujumbe wa Uislamu uko wazi wazi, wakijizatiti kwa kila aina ya vita kijeshi, kifikra, kithaqafa na kisheria ili kufikia lengo lao la kuizima kabisa nuru yake. Bila ya kusahau kuwa wao ndio wanaozuiya ulinganizi wa Uislamu kwa propaganda, kuuwa, kutesa, kupoteza na kuwasweka majela walinganizi mukhlisina kwa kisingizio cha sheria ya ubaguzi ya 'kupambana na ugaidi', na badala yake kuwatumia wakala wao waovu ambao huusaliti Uislamu kwa thamani duni ya maisha ya dunia.

Ibada ya Ramadhaani ni ibada tukufu yenye hadhi kubwa ndani ya Uislamu, haimaliziki tu katika upande wa utawa na kualikwa vyakula vitamu na wanademokrasia. Jambo hilo ni kinyume na ibada yenyewe, na pia ni kinyume na taarikh yetu tangu zama za Mtume SAAW, masahaba na wema waliofuatia. Wao waliuchukulia mwezi huu kuwa ni kipindi adhimu cha kukithirisha amali zote za kheri kuanzia swaum, sala za sunnah, usomaji wa Quran, kutoa sadaka, kufanya ulinganizi wa Uislamu, kupigana jihad dhidi ya makafiri na hata kufungua miji.

Ramadhani ndio mwezi wenye fungamano na jambo kubwa la msingi kwa ukombozi wa mwanadamu kwa kuanza ndani yake kushuka wahyi kwa Mtume SAAW. Kubwa zaidi pia Ramadhani ikateuliwa na Allah SWT kuwa ndio mwezi wa kushushwa muongozo wa Quran kutoka Bait -ul izzah mpaka kufikia wingu wa dunia. Kisha Quran kushushwa kidogo kidogo kufuatia matukio na minasaba mbalimbali kwa muda wa miaka 23 kupitia Mtume SAAW ili kwa muongozo huo awaongoze wanadamu wote.

Waislamu tuna wajibu wa kuchukua hadhari kubwa na mbinu na hadaa za maadui wa Uislamu ambazo ni hatari kwa Uislamu wetu na fikra zake. Aidha, tudharau dhihaka za mfumo wa kibepari na wafuasi wake. Bali tuzidishe shauku yetu kwa mgeni huyu mtukufu (Ramadhani) na kuyakumbatia kwa mikono miwili aliyokuja nayo kuanzia thamani ya kinafsia na ya kisiasa.

Na mwisho tukumbuke tuna jukumu kubwa la kulingania Uislamu kwa jitihada kubwa ili kuleta mageuzi kwa msingi wa Uislamu, ili mwaka ujao mgeni huyu Insha Allah apokewe na mwenyeji wa kheri, yaani dola ya Kiislamu ya Khilafah ambaye ndie mlinzi wa matukufu yote ya Kiislamu na Waislamu.

***********



## Mama Itumie Vyema Fursa ya Ramadhani


Allah *Ta'ala* amaemjaalia mama wa Kiislamu jukumu kubwa na adhimu linalowafikiana na maumbile yake la ulezi wa watoto, uangalizi wao na utunzaji wa nyumba yake. Pamoja na ukweli kwamba pia huruhusiwa (mubaha) kufanya kazi nyengine za halali nje ya nyumba yake bila ya kuathiri jukumu lake la msingi

Jukumu lake hilo la uangalizi wa nyumba na watoto humfanya mama kimaumbile kuwa na athari muhimu na ushawishi mkubwa ndani ya nyumba yake kwa watoto wake na mume wake kijumla. Kwa ufupi, mama huwa malkia ndani ya nyumba yake. Kwa hivyo, ni jambo la busara na fursa ya aina yake katika mwezi huu wa Ramadhani kwa mama wa Kiislamu kuutumia vyema ushawishi wake huo kwa lengo la kuhamasisha ibada, kuunga udugu na kuifikisha daawa ya Kiislamu kwa ujumla

Katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhan, mama atumie ushawishi wake kama mama, kwa watoto wake hususan watoto wake wadogo kwa kuanza kuwafundisha na kuwahamasisha kufunga Ramadhani kwa kuwapa moyo na kuwashawishi kwa zawadi ndogondogo ili waendelee kufunga. Hilo ni kutokana na ukweli kwamba Uislamu unatutaka tuanze kuwafundisha watoto wetu ibada mapema katika maisha yao, ili waweze kuzizoea ibada hizo katika umri wao wa mapema.

Na mama wa Kiislamu ana nafasi zaidi na ushawishi mkubwa zaidi kwa jambo hili.

Aidha, mama wa Kiislamu kwa kushirikiana na mumewe katika mwezi huu wa Ramdhani waitumie fursa kwa kuihamasisha familia yao kwa kila aina ya ibada kama swala za jam-



maa, tarewehe, swala za usiku, kutoa sadaka, kusoma Quran, kutembelea jamaa na kuhudhuria darsa na mihadhara mbalimbali ya kidini, na sio kuwaachia watoto kushiriki katika kuangalia michezo ya upuuzi katika Tv au kuutumia muda kwa michezo kama karata nk . Mama wa Kiislamu ana uwezo wa kulifanya hilo kwa ushawishi wake kama mama, na kutokana na kukaa kwake muda mwingi na watoto wake nyumbani.

Katika mwezi huu mtukufu, pia mama wa Kiislamu anaweza kuitumia fursa ya kuunga udugu zaidi, kwa kushauriana na mumewe kuwaalika ndugu na jamaa mbalimbali katika mwaliko wa futari kwa lengo la kuimarisha mahusiano zaidi ya kuunga udugu. Jambo hili la kuunga udugu ni ibada kubwa na miongoni mwa faradhi katika dini yetu.

Mwisho, mama wa Kiislamu aitumie fursa ya mwezi huu kwa kutekeleza jukumu kubwa, tukufu na faradhi la ulinganizi wa Kiislamu/daawa. Hili ni kwa kuwafafanulia ndugu, jamaa na marafiki ufaradhi wa kurejesha tena dola ya Kiislamu ya Khilafah Rashidah ambayo hutekeleza sheria zote za Kiislamu. Jukumu la ulinganizi ni la kila siku lakini kinamama wanaweza kuutumia usahali wa mwezi huu wa Ramadhani ambao nyoyo za Waislamu hujikurubisha zaidi kwa Allah *Ta'ala*.

Wanaweza kutumia mbinu mbalimbali na mbinu adhimu zaidi ni ya mwaliko wa chakula cha futari. Mbinu ambayo aliwahi kuitumia Mtume SAAW alipowaalika watu mbalimbali

mwaliko wa chakula ili kuwalingania Uislamu. Mbinu hii ni fursa muhimu ya kiurafiki na ya kimaumbile inayoweza kutumika kuwajenga Waislamu fikra thabiti juu ya Uislamu na kuasisi majadiliano ya kirafiki ili kuwaonesha ufaradhi wa kutawaliwa na dola ya Kiislamu ya Khilafah.

Ufanisi wa haya yote humpasa baba wa Kiislamu kuwa mstari wa mbele kwa kutoa mashirikiano yake kwa dhati. Kwa sababu majukumu hubebwa kwa mashirikiano ya baba na mama.

Allah *Ta'ala* anasema:

**وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنْ الْمُنكَرِ وَيُقِيمُونَ الصَّلاَةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُوْلَئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ**

*"Waumini wanaume na Waumini wanawake ni marafiki wao kwa wao. Huamrisha mema na kukataza maovu, na husimamisha Swala, na hutoa Zaka, na humtii Allah na Mtume wake. Hao Allah atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikma".* [TMQ 9:71]

********************



Hapa aya kwa muktadha wa nafasi ya Quran imetaja mambo mawili makubwa: Kwanza Quran ni muongozo, ubainifu na kipambanuzi. Pili, muongozo huo umelengwa kwa watu wote, kuna haja ya kujiuliza swali. Vipi Quran itakuwa muongozo kwa kafiri ambaye haiamini, haibebi wala haswali, hafanyi ibada ya Hijja wala hafungi? Inamuongozaje?

Qur'an itakuwa ikimuongoza kafiri kwa khiyari au kwa nguvu katika maisha yake katika upande wa kiutawala kuanzia uchumi, siasa, jamii, elimu nk. na sio katika upande wa ibdaat. Kwani makafiri licha ya kuwa hawalazimishwi kuwa Waislamu, lakini hutawaliwa juu yao na sheria za Kiislamu katika maisha yao ya kila siku chini ya Dola. Dola ya Kiislamu (Khilafah) ina wajibu kuwatawalia makafri wote kwa sheria za Kiislamu isipokuwa zile ambazo Uislamu umekuja kuzivua. Kama vile sheria za swala, swaum, hijja nk. Kwani ibada hizi kutekeleza kwake sharti msingi kwa mtekelezaji awe na imani ya Kiislamu, na wao makafiri hawana imani hiyo.

Hivi ndivyo alivyofanya Mtume (SAAW) katika kuamiliana na makafiri 'dhimmiy' na ndivyo vivyo hivyo wanavyofanya makafiri mabepari leo kuwalazimisha Waislamu kufuata sheria zao za maisha na kutubakishia mfumo wetu katika mambo ya kiroho tu kama funga, hijja, swala, ushauri nasaha katika masuala ya ndoa na mirathi (ukadhi) nk. Mfumo wa ubepari unayafanya haya, kwa kuwa hii ni moja katika sifa muhimu na ya lazima ya mfumo wowote. Sifa ya kulazimisha watu wote kuwa chini ya sheria na sera za mfumo unaotawala. Kwa kuwa Quran imeteremshwa katika mwezi huu wa Ramadhani ikiwa ni muongozo wa maisha wa wanadamu wote, maana yake ni wazi imekuja kutangaza kuwa Uislamu ni mfumo kamili wa maisha.

Tamko 'mfumo wa maisha' ni mwelekeo fulani rasmi wa kimaisha unaotokana na itikadi maalumu, na itikadi hiyo huzaa nidhamu mbalimbali za masuluhisho katika nyanja za elimu, siasa, jamii, uchumi, utawala, ibada nk. kwa ajili ya kutekelezwa chini ya utawala. Mfumo huo hutabikishwa kwa walioamini, na pia hutabikishwa hata kwa wasiouamini.

Ikiwa imani/dini imekosa nidhamu za maisha kutoka ndani ya imani hiyo. Dini hiyo huwa si mfumo wa maisha, bali inabakia kuwa dini tu. Kama zilivyo imani/dini za ukristo, uyahudi, ubaniyani, ubudha nk.ambazo hujihusisha na fungamano la mtu na Mola wake tu bila ya kuwa na masuluhisho yoyote katika maisha ya kila siku.

Kwa bahati mbaya kuna wanaotumia tamko hili la mfumo wa maisha wa Kiislamu, kwa maana finyu na isiyokamilika kinyume na inavyotakikana kufahamika na kulinganiwa kwa mujibu wa Uislamu.

Badhi huhubiri Uislamu kuwa ni mfumo kamili wa maisha, lakini mifano wanayoitoa bado haifikii maana halisi na pana ya tamko la mfumo wa maisha. Wengi huishia kutoa mifano ya namna ya Uislamu unavyofundisha kula, kunywa, kwenda haja, kuvaa nguo, kufanya jimai na dua kadhaa wa kadhaa. Kwa ufahamu wao huo wao huona hii ndio maana kamili ya kuwa Uislamu ni mfumo kamili wa maisha ya Muislamu tangu anapotoka usingizini, anaposhinda mchana mpaka anaporudi tena usiku kulala. Pamoja na ukweli kwamba hayo ni sehemu katika mfumo wa Kiislamu. Lakini bado haijakamillika maana halisi na pana ya tamko 'mfumo' kwa upana wake kwa kuwa hayakuhusisha sehemu muhimu ya uchumi, siasa za ndani, siasa za nje, vita, mahusiano ya mikataba na nchi za kikafiri, fedha ya nchi (sarafu) nk.

Huu ndio ufahamu wa nafasi ya muongozo na mfumo wake wa Kiislamu. Ndani ya mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ulioteremshwa Quran tuna umuhimu mkubwa kufafanua kwa kina kwa Ummah, ili uweze kushiriki kikamilifu kuurejesha tena maisha ya Kiislamu kwa kurejesha tena utawala wa Khilafah Rashidah.

*********

# FAT-HI YA ANDALUS

Moja miongoni mwa matukio ya Ramadhani ni ufunguzi/fathi wa Andalasia (Spain na Ureno). Chini ya Jemedari Tariq bin Ziyad aliyeongoza mapambano makali ndani ya mwezi wa Ramadhani mwaka 92 Hijiria/ 711 Miladiya. Mapambano hayo yalijiri ndani ya Ramadhani na kukamilika ndani ya mwezi wa Shawwal.

Twariq bin Ziyad alikuwa msaidizi wa Musa bin Naswir ambaye alikuwa ni Gavana wa eneo la Maghrib / Morocco. Jemedari huyo wa Kiislamu katika ufunguzi huo wa Andalusia alianzia na wanajeshi takribani 7000, kisha akaomba kuongezewa askari, na Gavana Musa bin Naswir akatuma idadi ya askari 5000 kwa merikabu wakiongozwa na Twarif bin Malik, hivyo idadi ya askari wa Kiislamu ikawa 12000.

Kwa upande wa makafiri wa Andalusia wao walikuja kwenye vita wakiwa na askari takriban laki moja, wengi wao wakiwa wamepanda vipando na silaha bora zaidi, wakiongozwa na Jemadari wao aliyejulikana kama Luthriiq aliyekuja katika medani ya vita akijifakhiri kwa kuvaa mavazi ya yaliyopambiwa maadini ya dhahabu na kipando chake kikikokotwa na nyumbu wawili.

Vita vilianza kupiganwa katika bonde la Burbat, eneo muhimu kistratejia ya kivita, nyuma yake kulikua na mlima mkubwa na upande mwingine ni sehemu ya bahari, ambapo kulikuwa na meli ambayo ndani yake kulikuwa na kikosi chini ya Jemadari Twaarif bin Malik.



Mapambano hayo yalidumu takriban siku nane, huku kukiwa na maiti na majeruhi wengi upande wa Waislamu, inakadiriwa takriban wanajeshi elfu tatu wa Kiislamu walipoteza maisha. Aidha, upande wa maadui kulishuhudiwa maelfu ya wanajeshi kuuwawa na kupatikana majeruhi wengi .

Mwisho wa mapambano hayo Mola SWT alijaalia nusra na ushindi upande wa Waislamu mwanzoni mwa mwezi wa Shawwal. Ama kiongozi wa Andalusia inasemekana aliuwawa, wengine wanasema alikimbia upande wa kaskazini mwa Andalusia, na utajo wake haukuwepo tena baada ya vita hivi. Katika vita hivi licha ya wapiganaji walikuwa na swaumu ya Ramadhani walipigana kwa uhodari mkubwa kwa msukumo wa uchamungu walioukuwa nao (Al-Bidayh Wanihayah, juzuu ya tisa uk. 138)

Ushindi huu wa Waislamu ndani ya Andalusia ukaleta nuru ya muongozo wa Quran nchini humo na kubadili maisha ya watu kwa kuwainua kifikra na kielimu, jambo lililoacha athari yake mpaka leo.

Aidha, ufunguzi huu ukafungua ukurasa mpya wa maendeleo makubwa ya kielimu na kiteknolojia. Vyuo vikuu vikubwa barani Ulaya vikajengwa katika miji ya Cordoba na Valencia vilivyokuwa chachu kubwa ya maendeleo.

Huo ndio utukufu wa Ramadhani, mwezi uliowasukuma Waislamu kuondoa kila aina ya kizuizi cha kufikisha nuru ya muongozo wa Quran na kutetea matukufu yao na kuufikisha ujumbe wa Uislamu mashariki na magharibi.

Hali hiyo kamwe haitajirudia mpaka pale yatakaporejea tena maisha ya Kiislamu chini ya utawala wa Khilafah Rashidah, ambapo dola hiyo itakomboa maeneo yote na kuufanya mwezi wa Ramadhani sio wa kula vinono tu, ilhali damu za Waislamu zikimwagwa, na matukufu ya Kiislamu yakidharauliwa.

Amesema Allah Taala :

"Na kama hivyo tumekufanyeni Umma bora (wasat) ili muwe mashahidi kwa watu na Mtume awe shahidi juu yenu"

***************



## Salamu za Amiri wa Hizb ut Tahrir kwa Kuanza Ramadhani 1447 H

Salamu ziwafikie Umma jumla, Umma bora uliotolewa kwa ajili ya wanadamu… Umma wa Kiislamu ambao Mwenyezi Mungu (swt) ameuutukuza kwa utiifu Kwake…

Pia salamu hizi ziende haswa kwa wabebaji wa Da'wah waheshimiwa ambao biashara wala kuuza kwao hakuwafanyi wasahau kumkumbuka Mwenyezi Mungu; Aliye Mtukufu kwa Uweza, Mwenye Hikima…

Vile vile salamu hizi ni kwa waheshimiwa wanaozuru ukurasa wangu wa Facebook wanaoifuata kheri inayobebwa na ukurasa huo.

Assalamu Alaikum wa Rahmatullahi wa Barakatuh,

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, na amani na baraka ziwe juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, juu ya ahli zake, maswahaba zake na wale wanaomfuata.

Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Akubali saumu na Qiyaam za Waislamu, na kwamba Mwenyezi Mungu (swt) Atusamehe madhambi yetu yote yaliyopita, kama alivyosema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) katika Hadith iliyopokewa na Bukhari na Muslim kwa riwaya ya Abu Hurayrah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alisema:

***«Mwenye kufunga Ramadhani kwa imani na kutarajia malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia.»***

Na katika riwaya nyingine Ndugu zangu waheshimiwa, katika mwezi wa Sha'ban wa mwaka wa pili baada ya Hijra, Mwenyezi Mungu Mtukufu alifaradhisha kufunga mwezi wa Ramadhani. Ni mwezi ambao Mwenyezi Mungu aliteremsha Qur'an:

***"Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa ndani yake Qur'an, kuwa ni uongozi kwa watu na hoja zilizo wazi za uongofu na upambanuzi." [Al-Baqara: 185].***

Ni mwezi ambao Mwenyezi Mungu aliuheshimisha Umma kwa ushindi na mafanikio makubwa kama vile Vita vikubwa ya Badr vilivyokuwa tarehe 17 Ramadhani ambapo washirikina wa Makka walishindwa kikamilifu… Kisha vikafuata vita vyengine vikubwa katika mwezi huu mtukufu, kuanzia na Ukombozi wa Makka tarehe 20 Ramadhani mwaka wa nane baada ya Hijra, hadi Vita vya al-Buwayb (karibu na mji wa Kufa kwa sasa) vilivyoitwa Yarmouk ya Waajemi ambapo Waislamu walishinda chini ya uongozi wa al-Muthanna tarehe 12 Ramadhani mwaka wa 13 H, kisha kufunguliwa kwa Amuriyah chini ya uongozi wa Al-Mu'tassim tarehe 17 Ramadhani mwaka wa 223 H, na Vita vya Ayn Jaloot ambapo Waislamu waliwashinda Watatari tarehe 25 Ramadhani mwaka wa 658 H, pamoja na ushindi mwingine katika mwezi huu mtukufu.

Basi ni kama hivyo saumu imefungamanishwa na Qur'an Tukufu, kitabu ambacho hakifikiwi na batili kutoka mbele yake wala nyuma yake… Vivo hivyo Saumu imefungamanishwa na ushindi na mafanikio makubwa…, Saumu imeunganishwa na jihad… Bali pia Saumu imeunganishwa na utekelezaji wa Sharia za Mwenyezi Mungu… Na mwenye uoni wa wazi aya za Mwenyezi Mungu, na anaye lingania kutenganisha Dini na maisha, au kutenganisha Dini na siasa, amefanya dhambi kubwa na kosa kubwa linalopelekea fedheha duniani na adhabu chungu Akhera.

Enyi Waislamu, ninawakumbusha haya katika siku hizi (za kuanza Ramadhani) ambazo uchokozi wa kikatili wa Mayahudi dhidi ya Ukingo wa Magharibi pamoja na Gaza unaendelea, na kisha uchokozi huo unaenea hadi Lebanon na Syria… mayahudi wanaingia wakitoka katika nchi za Kiislamu bila kukutana na upinzani wa kweli. Badala ya watawala hawa kuhamasisha majeshi ya Waislamu kupigana na dola ya Kiyahudi, kuwaondoa wanaoiunga mkono na kuikomboa Ardhi Iliyobarikiwa… tunawaona watawala hawa wakisaini makubaliano juu ya makubaliano na kijidola hicho cha mayahudi, na huku dhalimu Trump anawakusanya pamoja akiwadhalilisha, wakikosa haya mbele ya Mwenyezi Mungu, Mtume Wake au Waumini!

Hata hivyo, enyi Waislamu, kupambana dhidi ya Mayahudi, kuwaua na kuondoa kijidola chao lazima yawe chini ya uongozi wa Khalifah Rashidah ambaye ni mujahid wa kweli baada ya utawala huu wa dhulma na watawala vibaraka kuondoka.

Bishara njema ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) haitachelewa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu,

**naendelea uk 8**

## MATUKIO YA RAMADHANI

**1.Kupewa Utume Mtume (s.a.w)** Tarehe 18. Ramadhan – Kabla ya Hijra.

**2.Kufariki Abu Talib na Mama wa Waumini Bi Khadija [ra]** Kabla ya Hijra.

**3.Ushindi wa vita vya Badr,**Tarehe 17. Ramadhani – Mwaka wa 2. Hijria.

**4.Ghazwa ya Bani Salim,** Tarehe 28. Ramadhan, Mwaka wa 2.Hijria.

**5.Matayarisho ya vita vya Ahzab,** Mwaka wa 5. Hijria.

**6.Kutumwa kikosi cha Ghalib bin Abdillah Al-laith-** Kikosi hiki kilitumwa na askari 130 kwa kabila la Bani Awal na kabila la Abd bin Tha'labah. Ni katika tukio hili ndipo Usama bin Zaid alipomuuwa Mardas bin Nahik kimakosa (Mwaka wa 7AH)

7.Fathi Makka,**Tarehe 10.Ramadhani Mwaka wa 8.Hijria.**

**8.Kuanza kwa vita vya Tabuk ,**Mwaka wa 9. Hijria.

**9.Kusilimu kwa Msafara wa Ghuttan,**Mwaka wa 10. Hijria.

**10.Kufariki Abdallah bin Omar Al-khatab (r.a),** Mwaka wa 37. Hijria.

**11.Kuuwawa kwa Khalifah wa nne Ali ibin Abi Talib (r.a),** Mwaka 40. Hijria.

**12.Kufariki Amr Ibn Al-Ass [ra],** Mwaka wa 43. Hijria.

**13.Kufariki kwa Mama wa Waumini Bibi Aisha (r.a),** Mwaka wa 58. Hijria.

**14.Kutawazwa Ukhalifa kwa Abdul Malik bin Marwan,** Mwaka wa 65. Hijria.

**15.Fat-hi ya Spain (Andalusia) chini ya Tariq bin Ziyad.**(Mwaka wa 93. Hijria.)

**16Fat-hi ya Ommuriyah chini ya Khalifah Al- Mustasim.** (Mwaka wa 222. Hijria.)

**17.Fat-hi ya mji wa Babik Al-Kharm,** (Mwaka wa 222. Hijria.)

**18.Fat-hi ya Mji wa Sargosa- Sicily, (**Mwaka wa 264. Hijria.)

**19.Kujengwa kwa Azhar,** (Mwaka wa 361. Hijria.)

**20.Kuchukua Uongozi Abdulrahman bin Hisham ndani ya Cordoba- Spain,** ( 414. Hijria.)

**21. Jemadari Nurddin Al- Zinj awashinda wakiristo ndani ya mji wa Harem,** (559. Hijria.)

**22.Vita vya Hittin chini ya Salahudin Al Ayoub**.(Mwaka wa 584. Hijria.)

23. Vita vya Ain Jaloot ndani ya Palestina, **(Mwaka wa 627. Hijria.)**

24.Fat-hi ya mji wa Antakia- Syria, **(Mwaka wa 666. Hijria.)**

**25.Vita vya 'Balat Al Shuhadaa' 1st Ramadhan,** (Mwaka wa 1114. Hijria.)

**26.Kuibuka vita vya 'Harb Ramadhan'**(Mwaka wa 1392.Hijria.) 1948 Miladi

**27.Vita vya Suez Canal, 10 Ramadhan** [ Mwaka 1973 miladi].

**28. Mauwaji ya Waislamu yaliyofanywa na mayahudi ndani ya Masjid Ibrahim** [Al khalil] Hebron Palestina [1994 miladi]

**29.Vita vya Marekani ndani ya Afghanistan (**Mwaka 2002)

### Salamu za Amiri..uk 7

kama ilivyopokewa katika Hadithi ya Mtume (saw):

***"Kisha kutakuwa na utawala wa mabavu, utadumu kadiri Mwenyezi Mungu atakavyo, kisha atauondoa atakapopenda kuuondoa, kisha kutakuwa na Khilafah kwa Manhaj ya Unabii."***

Na pia kuthibitisha Hadithi:

***"Kwa hakika mtapigana na Mayahudi na mtawaua…" (Muslim)***

Kwa kumalizia, kama tunavyopaswa kuwa makini na saumu yetu ili Mwenyezi Mungu Aridhike nasi na Atusamehe madhambi yetu yaliyopita, basi pia tunapaswa kujitahidi kufanya kazi kwa ajili ya kurejesha mfumo wa maisha wa Kiislamu kwa kusimamisha tena Khilafah Rashidah ili tuwe miongoni mwa washindi katika dunia hii kwa utekelezaji wa Sheria za Mwenyezi Mungu, chini ya bendera ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), Rayat Al-Uqab, bendera ya La ilaha illa Allah Muhammad Rasul Allah, na pia tuwe miongoni mwa washindi Akhera, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, wale watakaopata kivuli Chake siku ambayo hakutakuwa na kivuli isipokuwa kivuli Chake, ili tupate ushindi katika makao yote mawili. Hakika huo ndio ushindi mkubwa.

Wassalamu Alaikum wa Rahmatullahi wa Barakatuh.

Ndugu yenu,

Sheikh Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah

Amiri wa Hizb ut Tahrir

1Ramadhani 1447 H / 18 Februari 2026 M